JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Fax:: +255 - 28-2810701
Phone: +255 -28-2810018
Mobile:
Email: kasulutc@moe.go.tz
Website: www.kasulutc.ac.tz

Chuo cha Ualimu Kasulu,
S.L.P 3,
KASULU

Kumb: Na. KACCU/GFO/77/VII/84 02/07/2020

Ndg;.....

S.L.P.....

.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA ASTASHAHADA/STASHAHADA 2020/2021

1. UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukuarifu rasmi kuwa; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Chuo cha Ualimu Kasulu kwa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada Maalumu Masomo ya Sayansi. Mafunzo haya ni ya miaka mitatu, **Hongera sana**. Aidha tunasisitiza kuwa uthamini uchaguzi huu kwa kusoma kwa bidii, kufuata taratibu na kanuni za Chuo kwa muda wote wa mafunzo uliopewa.

2. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo cha Ualimu Kasulu kipo Mkoa wa **KIGOMA** Wilaya ya **KASULU.** Kipo kilometa 92 kutoka Kigoma Mjini na kilomita moja kutoka standi kuu ya mabasi Kasulu. Ukifika stendi ya Mabasi Kasulu unaweza kufika kwa Mguu au kutumia usafiri wa Bodaboda kwa nauli ya Shilingi elfu moja tu.

3. KUFUNGUA CHUO

Chuo kitafunguliwa tarehe **24/08/2020** unatakiwa kufika chuoni ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kufungua chuo bila kukosa. Ukiwasili Chuoni fika ofisi ya **Usajili** ambapo utapokelewa na kupewa maelekezo. Iwapo hutafika tarehe **07/09/2020** Chuoni wiki mbili baada ya kufungua Chuo hutapokelewa.

4. WAKATI WA USAJILI UNATAKIWA UWE NA VITU VIFUATAVYO:-

i. Barua hii ya kuitwa kujiunga na Chuo (Joining instructions)
ii. Cheti halisi cha kumaliza kidato cha nne (School Leaving Certificate- Original).
iii. Cheti halisi cha kufuzu kidato cha nne (Academic Certificate of Secondary Education, O-Level) au Result Slip kwa wale waliomaliza mwaka 2018.
iv. Cheti cha kuzaliwa- Original.
v. Medical examination form iliyojazwa na Daktari wa Hospitari ya Serikali ya Wilaya.

5. VIFAA

i. Daftari na kalamu za kutosha, Mkebe wa Hisabati (Mathematical Instrument set).

ii. Rimu 1 (photocopy A4) karatasi rangi nyeupe, yenye karatasi 500.

iii. Mihtasari na Vitabu vya masomo yake ya kufundishia sekondari kidato cha I-IV angalau viwili.

iv. Mashuka mawili rangi ya pink (Wavulana) na light blue (Wasichana), blanketi 1, mto 1 na foronya 2 kwa ajili ya kulalia.

v. Vyombo vya kulia chakula: sahani 1, bakuli 1, kikombe 1, kijiko 1, galoni ya lita tano la plastiki kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.

vi. Nguo za michezo: tracksuit damu ya mzee fito tatu, bukta, soksi na raba kwa ajili ya siku za michezo. Mbali na sare ya chuo na nguo za michezo, Ualimu unahitaji mavazi ya heshima na nadhifu wakati wote, hivyo uje na mavazi yanayoendana na maadili ya ualimu muda wote.

6. ADA NA MICHANGO MBALIMBALI YA CHUO

(a) ADA YA MAFUNZO

Ada ya mafunzo ni **Tsh 450,000/=** kwa mwaka, hivyo kwa muhula unatakiwa kulipa **Tsh 225,000/=** ili usajiliwe. Ada utalipa kwa utaratibu wa **Control Number ya Wizara** ambayo utapewa na Mhasibu wa chuo baada ya kuripoti chuoni.

(b) MICHANGO MBALIMBALI

SN	MCHANGO	KIASI	MAONI
1	Serikali ya wanachuo	5,000	Kwa Mwaka
2	Huduma yakwanza	10,000	Kwa Mwaka
3	Usafi wa mazingira	20,000	Kwa Mwaka
4	Kukodisha godoro	10,000	Kwa Mwaka
5	Usajili na Kitambulisho	20,000	Kwa mwaka
6	Michezo	30,000	Kwa Mwaka
7	Ulinzi	30,000	Kwa Mwaka
8	Ukarabati	25,000	Kwa Mwaka
	JUMLA	**150,000**	

NB: Fedha ya michango yote ilipwe kwenye Akaunti ya Chuo **A/C 51403500048** Jina la akaunti ni **KASULU T.C. PROJECT, Benki ya NMB** kwenye tawi lolote, uje na BANK PAY SLIP.

7. SARE YA CHUO

Vazi rasmi la mwanachuo kwa muda wa masomo ni suti Uniform pair mbili **Kitambaa cha Dark blue ESTIMU NAMBA 1**. Na hakikisha inashonwa kama ilivyoelekezwa kuepuka kushona upya.

i. Suruali ya Dark blue (Wavulana). Upana uwe kati ya **16 – 18**, na iwe na turn up chini.

ii. Sketi ya Dark blue (Wasichana). Linda box mbele, Urefu ipite goti kabisa

iii. Koti dark blue kwa (Wote) na Tai rangi ya dark blue (Wote)

iv. Shati mikono mirefu light blue aina ya Kangaroo (Wote)

v. Viatu rangi nyeusi vya kufunika na kisigino kiwe kifupi kwa wote.

vi. Soksi Nyeupe kwa wasichana na Nyeusi kwa wavulana

vii. T-shirt light blue ya nembo ya Chuo yenye thamani ya Tshs 15,000/- itapatikana baada ya kufika chuoni.

viii. Koti refu jeupe kwa ajili ya kuvaa wakati wa mafunzo ya "Practical" wakiwa Maabara za masomo ya Sayansi.





8. CHAKULA NA AFYA

Chuo hutoa chakula kwa wanachuo wote. **Chuo hakina uwezo wa kutoa chakula maalumu (special diet)** kwa wagonjwa au mwanachuo mmoja mmoja, isipokuwa kitajitahidi kuboresha chakula kulingana na uwezo wake kifedha. Chuo hakitagharamia matibabu ya mwanachuo wakati wa mafunzo yake. Unatakiwa upimwe kwenye hospitali ya serikali iliyosajiliwa kuthibitisha afya yako kama inakuruhusu kuchukua mafunzo ya ualimu.

9. MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA YA WANACHUO

i. Mwanachuo anashauriwa awe na fedha tasilimu kwa ajili ya matumizi yake binafsi
ii. Mwanachuo mwenye kadi ya bima ya afya anatakiwa aje nayo. Asiye na kadi ya Bima ya afya aje na mchango wa kujiunga na mpango wa Bima ya afya ya Jamii (CHF) 50,400/=
iii. Mwanachuo anapaswa kufanya uchunguzi wa afya katika Hospitali za wilaya au mikoa kwa kutumia fomu iliyoambatishwa hapo chini.

NB: Mwanachuo ambaye hatakamilisha mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu hatapokelewa Chuoni.

MWISHO

Jumuiya ya Chuo cha Ualimu Kasulu inakutakia maandalizi mema ya safari ya kuja chuoni.

KARIBU SANA

HELLEN M. CHEYO
MKUU WA CHUO

NAKALA:
Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S. L. P 10,
DODOMA.

Mkurugenzi Msaidizi
Kitengo cha Mafunzo ya Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S. L .P 10`
DODOMA.

Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule (K)
Kanda ya Ziwa Magharibi
S.L.P 1185
KIGOMA

Afisa Elimu (M),
S.L. P 111
KIGOMA

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo,
S.L .P 3
KASULU

10. AMBATANISHO LA NAKALA YA SHERIA NA KANUNI ZA CHUO, NA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM

SHERIA NA KANUNI ZA CHUO:

Pamoja na maelekezo haya pokea sheria na kanuni za chuo ambazo utatakiwa kuzifuata wakati wote utakapokuwepo kwenye mafunzo, kama utaona ni ngumu kuzifuata ni bora usije kwa sababu ndizo zinazolinda na kuhifadhi amani na utulivu kwa lengo la kuwezesha kila mwanachuo kufikia malengo yaliyomleta hapa chuoni na taifa kwa ujumla.

1. Ni kosa kwa mwanachuo yeyote kutumia nafasi au uwezo wake kuwafanya wenzake au watu wengine wasitii Serikali halali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uongozi wa Chuo, Wakufunzi, Wafanyakazi wa chuo na serikali ya wanachuo. ADHABU: Endapo utavunja sheria hii utasimamishwa au kuachishwa mafunzo.

2. Kila mwanachuo anapokuwa nje ya mipaka ya chuo, ni LAZIMA awe na cheti cha ruhusa kinachotolewa na Mkufunzi wa zamu na awe amevaa sare ya chuo pamoja na kitambulishao cha chuo. ADHABU: Endapo utavunja sheria hii, utazuiliwa kutoka nje ya mipaka ya Chuo.

3. Ni marufuku kwenda nyumba starehe, nyumba za kulala wageni na nyumba za vileo. Aidha ni marufuku kutumia au kujishirikisha na madawa ya kulevya, uvutaji sigara/ bangi na kunywa pombe/vileo, pia ni kosa kushitakiwa kwa kosa lolote mahakamani. Endapo utavunja sheria hii utaachishwa mafunzo.

4. Inampasa kila mwanachuo kuheshimu kazi za mikono na afanye kazi kwa juhudi na maarifa, atumie muda wote uliopangwa kwa sababu, kufanya kazi ni sehemu ya mafunzo. Usipotimiza kanuni hii utaachishwa mafunzo.

5. Ni marufuku kupika bwenini, kwenda na chakula bwenini na kula chakula nje ya bwalo. Endapo utavunja sheria hii utasimamishwa au kuachishwa mafunzo.

6. Mwanachuo akidhoofisha afya yake kwa sababu ya uzembe au tabia chafu, akipata au kutoa mimba, wanachuo wakipeana mimba ata/watasimamishwa masomo na kufukuzwa chuoni. Mwanachuo akipatikana na mimba wakati wowote ataachishwa mafunzo mara moja.

7. Ni marufuku mwanachuo yeyote kumkaribisha mgeni katika mazingira ya chuo, bwenini, darasani, bwaloni au kumpatia chakula cha chuo bila idhini au kibali maalumu.

8. Mapambo na mavazi mbalimbali yanayokiuka misingi ya utamaduni wetu hayaruhusiwi kuvaliwa chuoni. Aidha kujigeuza rangi, kupaka rangi(wanja) , kuchuna na kuvaa nywele za bandia, kuacha masharafu/masharubu, ndevu, kuvaa mikufu , shanga, pete, bangili, mipira shingoni, unyoaji nywele mtindo wa panki au kipara haviruhusiwi. Kila mwanachuo awe nadhifu kwa mavazi, lugha na matendo mazuri wakati wowote. Adhabu: Kazi za jamii.

9. Ni marufuku mwanachuo kuwa na SIMU darasani, kwenye Baraza la Chuo au mikusanyiko rasmi inayofanyika ndani na nje ya Chuo. ADHABU:Endapo utavunja sheria hii utaachishwa mafunzo.

10. Ni marufuku kwa mwanachuo kuiba, kuharibu au kupoteza mali ya chuo au mtu mwingine yeyote. Adhabu: kulipa/ fidia, kusimamishwa masomo,kuachishwa mafunzo au adhabu zote kwa pamoja.

,GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

TO: The Medical Officer

From: Principal
Kasulu Teachers' College.

.....
.....

Please examine Mr/Mrs/Miss……..
To his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.

B: Blood Group

Date : ……..

Signature……
Official Stamp

.....

PART B: **MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time teacher Education course.

I. (a) Eye – sight……
(b) Hearing ……...
(c) Limbs……
(d) Speech…….
(e) Leprosy…….

II. Neuroses……

III. Other serious diseases……..

IV. Pregnancy……..

Name of Medical officer .....Signature.....

Date: ..... **Official Stamp**